JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## WITO KWA WATAALAMU: KUUNDA MUSTAKABALI WA KIJAMII NA KIDIJITI KWA MIJI NA MAJENGO

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu umma kuwa imepokea fursa kutoka Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU) kwa Watanzania kushiriki katika mpango wa kimataifa unaojulikana kama "**United for Smart Sustainable Cities (U4SSC)**." **U4SSC** ni mpango unaoratibiwa na ITU kwa shabaha ya kutafuta masuluhisho yenye ubunifu kwa maendeleo endelevu ya mipango miji. Hivyo wataalam wa mipango miji, uhandisi, sayansi ya jamii, utawala wa umma na taaluma nyingine wanaalikwa kushiriki na kutoa utaalamu wao ili kuchangia mafanikio ya mpango huu.

**Mpango huu umegawanyika katika makundi yafuatayo:**

**1. Utawala wa Miji Unaolenga Watu na Ustahimilivu wa Kijamii na Utamaduni**
Kundi hili linalenga kuunganisha vipaumbele vya kijamii katika maamuzi ya uundaji wa zana ya kidijiti ili kusaidia mipango miji na kuweka uwiano wa ustawi wa jamii, ukuaji wa uchumi na uangalizi wa mazingira. Kwa maelezo zaidi kuhusu kundi hili, tafadhali tembelea kiunganishi kifuatacho: https://u4ssc.itu.int/social-cultural-sustainability

**2. Mabadiliko Endelevu wa Kidijiti kwa Mipango Miji katika Ujenzi na Nishati**
Kundi hili litazingatia kuongeza ufanisi wa rasilimali, kuhamasisha ubunifu katika mifumo ya nishati mijini na kukuza mipango ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia teknolojia za kidijiti. Kwa maelezo zaidi kuhusu kundi hili, tafadhali tembelea kiunganishi kifuatacho:**https://u4ssc.itu.int/buildings-and-energy**

Anayetaka kushiriki katika mpango huu anatakiwa kutembelea viunganishi tajwa hapo juu na kuwasiliana na U4SSC kupitia baruapepe: **u4ssc@itu.int**. Pindi atakapojiunga katika mpango huu, anatakiwa kuitaarifu TCRA kupitia **dg@tcra.go.tz**.

Imetolewa Tarehe **06 Aprili, 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Sun Apr 06 14:58:41 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**